

The
Management
University
of Africa



Sponsored by the Kenya Institute of Management

UNDERGRADUATE UNIVERSITY EXAMINATIONS

SCHOOL OF MANAGEMENT AND LEADERSHIP

DEGREE OF BACHELOR OF EDUCATION ARTS

KIS 318: MBINU ZA KUFUNDISHA

TAREHE: 10TH APRIL 2026

MUDA: MASAA MAWILI

JUMLA YA ALAMA: 70

MAAGIZO:

1. Andika nambari yako ya usajili katika kitabu cha majibu ulichopewa.
2. **USIANDIKE CHOCHOTE** kwenye karatasi ya maswali
3. Karatasi hii ya mtihani ina maswali **sita (6)**
4. **SWALI LA KWANZA** ni la lazima
5. Jibu maswali mengine **MATATU** kutoka sehemu zilizobaki.
6. **SWALI LA KWANZA** lina alama **25** ilhali maswali mengine yana **ALAMA 15** kila moja.
7. Jibu majibu yako yote katika kitabu cha majibu/ mtihani ulichopewa.

SWALI LA KWANZA

- a) Fafanua mikakati saba ambayo imewekwa ili kustawisha maenezi ya Kiswahili nchini Kenya. **(alama 07)**
- b) Jadili vizuizi kumi ambavyo vinaweza kuathiri kusikiza kwa ufahamu. **(alama 10)**
- c) Tambulisha shabaha nane za somo la Kusikiliza na Kuongea. **(alama 08)**

SWALI LA PILI

- a) Ni nini umuhimu wa silabasi **(alama 07)**
- b) Jadili madhara ya kukosa maandalizi mwafaka kwa mwalimu wa lugha. **(alama 08)**

SWALI LA TATU

- a) Katika kufundisha tamthilia, tambua vigezo vya uchambuzi wa kifasihi utakavyozingatia katika kufanikisha somo hili. **(alama 06)**
- b) Andaa mpangilio wa kipindi wa somo kuhusu mada uipendayo litakalochukua dakika 40. **(alama 09)**

SWALI LA NNE

- a) Fafanua malengo saba ya kufundisha Lugha ya Kiswahili nchini Kenya. **(alama 07)**
- b) Pambanua umuhimu wa mbinu ya mdahalo katika kufundisha wanafunzi lugha. **(alama 08)**

SWALI LA TANO

Huku ukitoa mifano mwafaka, jadili sifa, ubora na upungufu wa mbinu ya maigizo katika kufundishia fasihi simulizi. **(alama 15)**

SWALI LA SITA

- a) Pambanua njia tano ambazo zinaweza kutumika katika kuleta mvuto wakati wa kusoma ushairi. **(alama 05)**
- b) Jadili vigezo vitano ambayo hutumiwa katika kuchambua ushairi. **(alama 10)**